TANGAZO LA SERIKALI NA. 274 la tarehe 12/4/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

**SHERIA NDOGO**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE YA MWAKA 2024

Jina TS. Na 808 la tarehe 2019

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ya Mwaka 2024, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ya Mwaka 2019, ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 11

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 11 kama ifuatavyo:

"Ukataji na uvunaji Miti

11.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kukata au kuvuna miti kwa ajili ya matumizi ya aina yeyote bila kibali cha Halmashauri au Wakala wa Huduma za Misitu.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kuwa na msumeno wa moto bila kupata kibali cha Halmashauri au Wakala wa Huduma za Misitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata au kuvuna miti au nyasi katika eneo la mlima, bonde, korongo au chanzo cha maji.

(4) Mtu yeyote aliyepata kibali kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atawajibika

kuhakikisha kuwa anakata miti kwa mujibu wa kibali husika."

Marekebisho ya kanuni ya 12

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 12 kwa kuongeza aya ndogo ya (3) kama ifuatavyo:

"(3) Kila mmiliki au mpangaji wa nyumba au kiwanja kilichopo mjini atalazimika kupanda na kutunza miti isiyopungua mitano, na kwa nyumba, kiwanja au shamba lililopo kijijini atalazimika kupanda na kutunza miti isiyopungua kumi."

Marekebisho ya kanuni ya 20

4. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 20 kwa kuongeza aya ya 13 kama ifuatavyo:

"(13) ataingiza mifugo katika eneo ambalo limezuiliwa kufanyika shughuli za uchungaji au kuingiza mifugo katika mashamba".

Marekebisho ya kanuni ya 22

5. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 22 kama ifuatavyo:

"Adhabu

22. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.".

Lakari ya Halmashauri ya wilaya ya Songwe iliyogongwa katika Sheria Ndogo hizi kwa kufutia Azimio Na SDC/ MB/09/2023 la Kikao cha Halmashauri ya Wilaya Songwe cha Tarehe 02/1/2023 na imebaandikwa na kushuhudiwa mbele ya;-

CPA CECILIA D KAVISHE
*Mkurugenzi Mtandaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Songwe*

ABRAHIM KAGULUKA SAMBILA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Songwe*

L.S

NAKUBALI

Dodoma,
31 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*